JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

**SHAURI NA. 07 - 2018/2019**

**AZAM MEDIA LTD**

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

## 1.0 Utangulizi

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa maudhui mtandaoni kwa **Azam Media Ltd**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni. Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yo yote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.2 Tarehe 14 Aprili, 2019, **Azam Media Ltd.,** kupitia chanel yake iliyopo Youtube, instagram na Facebook ilichapisha na kuweka maudhui yanayolidhalilisha kabila la Wamasai, yenye kichwa cha habari **Wamasai Hutumia Mkojo Wa Binadamu Kujenga Nyumba Zao**:

1.3 Maudhui hayo ya picha jongefu yalirushwa katika kipindi cha **Makabila** na kueleza kwamba Wamasai hutumia mkojo wa binadamu, kinyesi cha ng'ombe, majivu, matope, vijiti na majani wakati wa kujenga nyumba zao.

1.4 Maudhui hayo yalirushwa bila kuzingatia weledi wa uandishi wa habari na kuipotosha jamii kwa sababu hakuna vyanzo vya habari au utafiti wo wote ulioonyeshwa katika taarifa hiyo kuthibitisha kwamba Wamasai hutumia mkojo wa binadamu kujenga nyumba zao.

1.5 Katika picha jongefu hiyo, mtangazaji wa kipindi alitamka maneno yafuatayo: ***Usilolijua kuhusu nyumba za Wamasai ni kwamba hutumia mkojo wa binadamu, kinyesi cha ng'ombe, majivu, matope, vijiti, na majani kujenga nyumba zao....*** *"Wamasai ni moja kati ya watu wa jamii ya wanaohamahama hivyo hata makazi yao huwa si ya kudumu na hujenga nyumba zao kirahisi. Nyumba za kimasai zina umbo la nyota au mviringo na hujengwa na wanawake. Ujenzi wa makazi haya hutumia mbao na matawi madogo yaliyochanganywa na matope, vijiti, majani, kinyesi cha ng'ombe na mkojo wa binadamu pamoja na majivu. Mchanganyiko huu husaidia paa za nyumba zao kutovuja kipindi cha mvua. Licha ya hivi sasa mambo yamekuwa tofauti kuna baadhi huezeka nyumba zao kwa bati."*

1.6 Kitendo cha kuweka picha jongefu yenye maudhui ya upotoshaji, uongo na yanayoiudhi jamii ya kimasai, **Azam Media Ltd** imekiuka Kanuni Na. 5(1) (a), (b), 5 (2) (b), na 12 (l) (iii) na 12(h) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018 zinazomtaka kila mtumiaji wa mitandao ya kijamii kutochapisha taarifa za uongo zitakazoipotosha, kuidanganya au kuisirisha jamii. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo;

5 (1) *For the purpose of these Regulations, an online content provider shall*

*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

*(b) take into account trends and cultural sensitivities of the general public;*

5 (2) *A subscriber and user of online content services shall;*
*(b) ensure his posts do not contravene the provisions of these Regulations and any other written law.*

12. *Online content service provider shall not publish;*
(I) *false content which is likely to mislead or deceive the public unless where it is clearly pre-stated that the content is;*

(iii) *where it is preceded by a statement that the content is not factual.*

*(h) content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime, or leads to public disorder.*

## 2.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui.

Tarehe 22 Mei, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Azam Media Ltd** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 3 Juni, 2019, uongozi wa **Azam Media Ltd** ukiongozwa na **Bw. Tido Mhando**, Mtendaji Mkuu (CEO) wa Azam Media Ltd, aliyeambatana na Bw. Yahya Mohamed, Mkurugenzi wa Vipindi, Bi. Happiness Sedoyeka, Meneja wa Utayarishaji wa Vipindi vya TV, na Bw. Hassan Mhelela, Mhahiri wa Maudhui Mitandaoni ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wake.

## 3.0 Kusikiliza na Kuangalia Maudhui Mitandaoni ya Azam Media Ltd.

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Azam Media Ltd** walisikiliza na kuangalia maudhui mtandaoni ya tarehe 14 Aprili, 2019 yaliyochapishwa na **Azam Media Ltd** katika chaneli yake iliyopo katika mtandao wa Youtube na katika mitandao ya kijamii ya Instagram na Facebook ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 4.0 Maelezo ya Utetezi ya Azam Media Ltd.

Uongozi wa **Azam Media Ltd** ulikiri kuchapisha maudhui yaliyokuwa na kichwa cha habari, **"Wamasai hutumia Mkojo wa Binadamu Kujenga Nyumba zao"** na pia uliomba radhi kwa kuwaudhi na kuwakera watumiaji wa mitandao ya kijamii kupitia maudhui hayo.Uongozi ulisema kwamba haikuwa dhamira yao kuwaudhi na kuwakera watazamaji wao kwa kuwa kipindi chao kililenga kuchapisha/kuweka maudhui ambayo yalilenga kuibua mila za kitanzania zilizosahaulika.

Uongozi ulidai kuwa maudhui yaliyochapishwa yalitokana na rejea za tafiti mbali mbali ambazo watayarishaji wa kipindi walizipata kutoka kwenye vitabu na machapisho yanayopatikana mitandaoni kupitia "*search engine*" yakielezea tamaduni za kabila la Wamasai ikiwemo mbinu ya ujenzi wa nyumba kwa kutumia mkojo wa wanyama na wakati mwingine mkojo wa binadamu. Ulizidi kudai kuwa maelezo hayo pia yalipatikana kutoka kwa mmoja wa viongozi wa Kimasai aliyezungumza na waandaaji wa kipindi "*off the camera*".

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa Azam Media Ltd. pia uliikabidhi Kamati nakala za tafiti na "link" za mitandao ya wavuti ambazo zina machapisho yenye maudhui hayo.

4.1 **Bw. Tido Mhando** aliomba radhi kwa makosa waliyoyafanya katika uzalishaji wa kipindi chao kwa kushindwa kuwahoji Wamasai wenyewe kuhusu uhalisia wa maudhui hayo; kushindwa kuchapisha nukuu ya vitabu na machapisho ambayo walidai ndiko walioyatoa maudhui hayo; pamoja na kushindwa kutumia lugha ya staha katika kuchapisha maudhui yenyewe.

## 5.0 Majumuisho ya Utetezi wa Azam Media Ltd.

Katika kujumuisha utetezi wao, **Bw. Tido Mhando** aliendelea kuomba radhi na kusema kuwa **Azam Media Ltd** iko tayari kupokea maelekezo ya njia bora ya kuendelea kutoa maudhui yao mitandaoni bila ya kuvunja Sheria na Kanuni.

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Kamati imepokea tamko la Azam Media Ltd, la kukiri kosa na Kuomba radhi.

6.2 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Azam Media Ltd.** Imetenda kosa la kuchapisha mitandaoni maudhui yasiyo na mizania kwa kushindwa kuwahoji Wamasai wenyewe au kubainisha chanzo chao cha maudhui, kuchapisha maudhui yanayoudhi na ambayo hayakutumia lugha ya staha kinyume na Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji.

6.3 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa utetezi wa **Azam Media Ltd.** hauna uzito wa kitaaluma na kwamba maudhui iliyochapisha hayakuzingatia uhalisia, weledi, uadilifu, na wala hayakuwa na nukuu kutoka chanzo chake.

## 7.0 Ushauri wa Kamati kwa Azam Media Ltd.

Kamati haia nia ya kudhibiti ubunifu wa Watangazaji wetu nchini bali kuboresha kitaalamu Maudhui ya Vyombo vyao. Kamati inawaasaa Watangazaji kuzingatia weledi Sheria, Kanuni na Maadili ya Tasina.

Hata hivyo, kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Azam Media Ltd** kuimarisha na kuzingatia usimamizi na uhariri makini wa vipindi vyao ili kuhakikisha kuwa maudhui yao yanafaa kabla ya kuwekwa mitandaoni.

## 8.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Azam Media Ltd**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Azam Media Ltd** kupitia chaneli yake iliyopo katika mtandao wa kijamii wa Youtube na katika mitandao ya Instagram na Facebook imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

**Hivyo basi**, Kamati ya Maudhui imeamua yafuatayo:

**Azam Media Ltd.** kulipa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018;

Pamoja na faini hiyo **Azam Media Ltd.** inapewa Onyo Kali na, pia ina aamriwa kuomba radhi kwa Watanzania kwa kosa lililofanyika kupitia chaneli yao ya Youtube na katika mitandao ya kijamii ya Instagram na Facebook kwa siku saba (7) mfululizo kuanzia tarehe 05/06/2019;

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **04** mwezi **Juni** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeneingo-Sia Msoka**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

......................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ........................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**....................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**.........................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**...........................................